**Nambari ya Mtahiniwa ________________**

**SMZ**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA**

**126** **HISTORIA**

**MUDA: SAA 2.00** **IJUMAA 29 OKTOBA, 2021 MCHANA**

---

**MAELEKEZO KWA WATAHINIWA**

1. **Mtihani huu una sehemu TATU (3) A, B na C.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Jibu maswali MANNE (4) kutoka sehemu C.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
5. **Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
6. **Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| **NAMBARI YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI** |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| JUMLA | | |

**Mtihani huu una kurasa 14 zenye maandishi**

**Nambari ya Mtahiniwa ________________**

## SEHEMU A: (Alama 20)

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. Chagua jawabu sahihi na uandike herufi yake katika jadweli lililopo hapo chini.

i. William Mackinon alianzisha Kampuni ipi kati ya zifuatazo?

A. British East African Company B. British South African Company
C. German East African Company D. Royal Niger Company

ii. Ni nani aliyekuwa rais wa Zanzibar kuanzia mwaka 1985 hadi mwaka 1990?

A. Mh. Aboud Jumbe Mwinyi B. Mh. Amani Abeid Karume
C. Mh. Idris Abdul Wakil D. Mh. Salmin Amour Juma

iii. Mapinduzi ya Zanzibar yalitokea tarehe gani?

A. 10/01/1964 B. 11/01/1964
C. 12/01/1964 D. 13/01/1964

iv. Kati ya wafuataо ni yupi aliyekuwa mwanzilishi wa mfumo wa utawala usio wa moja kwa moja barani Africa?

A. Donald Cameroon B. Edward Twinning
C. Friedrick Lurgard D. Richard Tumbull

v. Ipi kati ya zifuatazo ni orodha sahihi ya wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

A. Tanzania, Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe na Malawi
B. Zambia, Sudan, Uganda, Congo, Mozambique na Tanzania
C. Congo, Malawi, Uganda, Rwanda, Zambia na Chad
D. Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan

vi. Mkataba wa Heligoland ulisainiwa mwaka gani?

A. 1878 B. 1880 C. 1899 D. 1890

vii. Ipi kati ya zifuatazo **haikuwa** sekta kuu za uchumi wa kikoloni?

A. Kilimo B. Benki C . Uchimbaji madini D. Ufugaji

viii. Tippu Tip, mfanya biashara maarufu wa watumwa, jina lake halisi anaitwa nani?

A. Barghash bin Said Al-Busaid
B. Juan Bautista de Anza
C. Hamad bin Muhammad bin Juma
D. Hassan Ahmed Bin Ahmed

ix. Chama cha TANU kilitokana na mabadiliko ya chama gani?

A. ASP
B. TAA
C. TTCSA
D. ZAA

x. Makao makuu ya SADC yako katika nchi gani?

A. Abuja, Nigeria
B. Arusha, Tanzania
C. Bujumbura, Burundi
D. Gaborone, Botswana

**JAWABU**

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Andika **KWELI** kwa maelezo sahihi au **SIKWELI** kwa maelezo yasiyo sahihi katika jadweli lililopo hapo chini.

i. Wakati wa kupigania Uhuru, Zanzibar ilikuwa na chama kimoja tu cha siasa.
ii. Zanzibar iliwahi kutawaliwa na Wajerumani.
iii. Chama cha TANU kilikabiliwa na changamoto ya fedha wakati wa kupigania uhuru.
iv. Uingereza ilikuwa ndio taifa la kwanza kuitawala Tanganyika.
v. USSR iliunga mkono kuanzishwa kwa mfumo wa chama kimoja barani Afrika.
vi. Wakati wa Ukoloni huduma ya afya ilitolewa kwa kuzingatia rangi, jinsia na dini.
vii. Zimbabwe ilipata uhuru tarehe 18/04/1978.
viii. Gambia, Ivory Coast na Liberia ni miongoni mwa nchi wanachama wa ECOWAS.
ix. Katika mfumo wa ujima hakukuwa na umiliki wa ardhi kwa mtu binafsi.
x. Vita vya msituni nchini Msumbiji vilianza mwaka 1964.

**JAWABU**

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

Nambari ya Mtahiniwa _______________

## SEHEMU B: (Alama 40)

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

3. Chagua jawabu sahihi kutoka **KIFUNGU B** inayokubaliana na maelezo ya **KIFUNGU A**. Andika herufi ya jawabu ndani ya jadweli lililopo hapo chini.

| KIFUNGU A | KIFUNGU B |
|---|---|
| i. Mkutano wa Berlin | a. Mwanasiasa na Mwanamapinduzi wa Ghana |
| ii. Mkataba wa Heligoland | b. Uliandaliwa na Patrice Lumumba |
| iii. ASP | c. Kilianzishwa mwaka 1954 |
| iv. Kwame Nkrumah | d. Ulisainiwa kati ya Ujerumani na Uingereza |
| v. ZNP | e. Kilianzishwa mwaka 1957 |
| | f. Uliandaliwa na Otto Von Bismarck |
| | g. Ulisainiwa kati ya Uingereza na Ufaransa |
| | h. Ulisainiwa mnamo Septemba 1822 |

**JAWABU**

| i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

4. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika jibu sahihi ulilopewa chini ya jadweli

| Jina la sasa | Jina la zamani |
|---|---|
| a. Ghana | _______________ |
| b. _______________ | Northern Rhodesia |
| c. Malawi | _______________ |
| d. _______________ | Basutoland |
| e. Burkina Faso | _______________ |
| **Zambia, Ivory coast, Upper Volta, Gold Coast, Msumbiji, Nyasaland, Lesotho** | |

5. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.

a) Orodhesha sifa mbili (2) za mfumo wa uzalishaji wa Ukabaila.

i. ______________________________

ii. ______________________________

b) Andika kirefu cha maneno yafuatayo.

i. AMNUT ______________________________

ii. ZPPP ______________________________

c) Taja tofauti mbili (2) kati ya mfumo wa utawala wa moja kwa moja na ule usio wa moja kwa moja.

i. ______________________________

ii. ______________________________

d) Bainisha madai mawili (2) ambayo umoja wa Basukuma uliyapigania mwaka 1938 katika harakati za awali za kudai uhuru Zanzibar.

i. ______________________________

ii. ______________________________

e) Taja Jumuiya mbili (2) za kimataifa ambazo ziliunga mkono harakati za kudai uhuru nchini Zimbabwe.

i. ______________________________

ii. ______________________________

**SEHEMU C: (Alama 40)**

**Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii.**

6. Elezea changamoto nne (4) zilizoikabili nchi ya Msumbiji wakati wa kupigania Uhuru wake.

______________________________

______________________________

______________________________

7. Chambua malengo manne (4) makuu ya kuanzishwa kwa Chama cha Afro-Shirazi Zanzibar.

8. Fafanua sababu nne (4) zilizopelekea uvamizi wa kikoloni Zanzibar.

9. a) Nini maana ya elimu ya kikoloni?

b) Chambua athari hasi nne (4) za elimu ya kikoloni katika nchi za Afrika.

10. Eleza kwa kifupi athari nne (4) hasi za uchumi wa kikoloni kwa jamii za Waafrika.

11. Onesha faida nne (4) za mfumo wa vyama vingi katika nchi za Afrika.

-----------------------------------